# NJIA YA MAFANIKIO KWA KIJANA MKRISTO



## MAADILI YA NENO LA MUNGU

Ukundi Nkya Sillo

**Mawasiliano na Mwandishi**

Simu: 0784 763 131

Email: ukundinkyaj@gmail.com

**Toleo la 1: November 2019**

**ISBN:987-9976-5485-9-4**

**Kimechapishwa na**

**Truth Printing**

**0764 425 704/ 0652 383 590**

geofreymakula@gmail.com

**Dar es salaam Tanzania**

## YALIYOMO


UTANGULIZI....................................................................4

ISAFISHE NJIA YAKO........................................................ 4

SURA YA KWANZA...........................................................7

MUNGU ANAYAPENDA MAFANIKIO YAKO..................7

SURA YA PILI..................................................................15

ANZA KWA KUJITAMBUA.............................................15

SURA YA TATU...............................................................27

CHAGUA MAADILI YAKO KWA HEKIMA......................... 27

SURA YA NNE.................................................................. 36

MAADILI YALIYOHAKIKISHWA...................................... 36

SURA YA TANO.................................................................. 43

AMUA KUWA KIELELEZO KWA MAISHA YA MAFANIKIO.........................................................................43

KIELELEZO KATIKA USEMI *(IN SPEECH)*...............48

KIELELEZO KATIKA MWENENDO *(IN CONDUCT)*56

UWE KIELELEZO KATIKA UPENDO..........................75

*(IN LOVE)*.................................................................... 75

UWE KIELELEZO KATIKA IMANI................................ 88

*(IN FAITH)*.................................................................... 88

UWE KIELELEZO KATIKA USAFI..............................102

(IN PURITY)...............................................................102

HITIMISHO ……………………………………….121

# UTANGULIZI

## ISAFISHE NJIA YAKO

Mpendwa mtoto wetu na kijana wetu katika kanisa la Mungu, ninakusalimu kwa Jina la BWANA na MWOKOZI wetu YESU KRISTO.

Ninamshukuru MUNGU kwa nafasi aliyonipa ya kuzungumza na wewe kwa njia ya maandishi kuhusu somo hili muhimu lenye LENGO la kukuandaa ili upate kuishi maisha yako kwa mafanikio zaidi. Maisha ya mafanikio ni yale yatakayokuletea furaha na amani mbele za Mungu na mbele za wanadamu. Ili kuyafikia mafanikio hayo ni lazima uwe mtu unayejitambua na kujithamini na mwenye kujisimamia ili usiangukie katika mtego na hila za adui shetani. Ninaamini UTAFANIKIWA ikiwa utazingatia mafundisho haya pamoja na mengine mema unayofundishwa nyumbani, shuleni na kanisani.

Ninaamini MUNGU amekupa wazazi na walezi wazuri ambao wamekuwa wakikufundisha na hata kukupeleka katika nyumba ya BWANA ili upate kufundishwa NENO la MUNGU. Kwa hili unapaswa kumshukuru sana Mungu. Usisahau kwamba wapo watoto wengine wengi ambao hawakupata neema uliyoipata wewe, na kwa sababu hiyo wamekosa mambo mengi mema ambayo wewe umefundishwa. Ninakuomba utakapokutana na watoto wa aina hiyo, fanyika baraka kwao kwa kuwashirikisha mema uliyo nayo ili na wao wapate neema ya kumjua Mungu wao.

Ninamshukuru MUNGU kwa ajili ya uongozi wa kanisa kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwafundisha watoto NENO la MUNGU, kuanzia madarasa ya **“Sunday school”** na pia madarasa ya “**kipaimara”**. Mimi ni zao zuri la madarasa hayo na nimeona jinsi masomo niliyofundishwa wakati huo yalivyofanyika msingi imara wa imani yangu. Kipekee ninawashukuru waalimu wanaojitoa kwa moyo kuwafundisha watoto NENO la MUNGU katika madarasa hayo yote. Mungu awabariki na awawezeshe kuufikia utukufu ule Mkuu waliowekewa mbele yao.

Kijana wetu mpendwa katika kanisa la Mungu; ninakuomba katika kuienzi kazi njema inayofanywa na watumishi wa Mungu, kubali kuyatumia vizuri mafundisho yote mema uliyopata ili uyafanikishe maisha yako na kufanyika baraka kwa kanisa na kwa taifa letu. Ni vema ukatambua kwamba wewe ni mtu muhimu sana mbele za Mungu na mbele ya watu wote. Matazamio yetu ya baadaye ni wewe uwe miongoni mwa watakaokuwa viongozi wetu katika nyanja mbalimbali katika taifa na katika kanisa; Na tena uwe miongoni mwa wataalamu katika maeneo mbalimbali kama vile udaktari, uandisi, ualimu, mshauri, mfanya biashara, mkulima mkubwa na hata katika nyanja nyingine ambazo hazijatajwa hapa. Zaidi ya yote unatazamiwa kufanyika baba au mama bora utakayeijenga familia bora kwa utukufu wa Jina la YESU. Yote hayo yatafanikiwa ikiwa utajitoa kuisafisha njia yako sawasawa na NENO la

Mungu. Imeandikwa;

***“Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako”; Zaburi 119:9***

Ninakuombea Roho Mtakatifu akuwezeshe kuona umuhimu wa kujijengea maadili mema ndani yako kwa kutii na kulifuata Neno la MUNGU, ili ufanikiwe kimaisha kwa utukufu wa Jina la YESU.

**MUNGU AKUBARIKI SANA**

**Mtumishi wa Kristo,**

**Ukundi Nkya Sillo.**

# SURA YA KWANZA

## MUNGU ANAYAPENDA MAFANIKIO YAKO

Mpendwa mtoto wetu na kijana wetu katika kanisa la Mungu; ninaamini unapenda kufanikiwa na kuwa na maisha mazuri ya amani na furaha. Ukweli ni kwamba kila mtu anapenda kufanikiwa na kuwa na maisha mazuri. *Hebu tafadhali tulia kidogo, funga macho na ndani ya moyo wako jaribu kupiga picha ya maisha yako miaka kama ishirini ijayo. Ninaamini unajiona mwenye afya njema, familia nzuri, kazi nzuri, furaha amani na upendo.* Ni maono mazuri na yenye kutia moyo sana. Kutamani kuwa na maisha mazuri ni jambo jema. Lakini siyo wewe tu unayetamani uje kuwa na maisha mazuri bali hata wazazi wako, waalimu na viongozi wako wote pia wangependa uje kufanikiwa kimaisha. Cha kufurahisha zaidi ni kwamba MUNGU naye anapenda ufanikiwe na uwe na maisha mazuri yanayompendeza Yeye. Imeandikwa;

***Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo. 3 Yohana 1:2.***

Pamoja na kwamba watu wote tunapenda mafanikio haimaanishi wote tumefanikiwa au tutafanikiwa. Zipo sababu nyingi zinazochangia kumfanya mtu awe na mafanikio au asifanikiwe kimaisha. Sababu hizo zinaweza kuwa za kimaadili, kiimani na kimazingira. Wapo watu ambao kutokana na mazingira waliyozaliwa

na kulelewa wanakosa fursa na miongozo muhimu ya kuwawezesha kufanikiwa. Wapo wengine ambao wamejenga maadili yao juu ya msingi mbaya usio na nguvu ya kubeba mafanikio. Tena wapo ambao kutokana na kukosa IMANI katika uweza wa MUNGU wa kuwafungua wameendelea kukaa katika vifungo vya shetani vinavyowazuia wasifikie mafanikio yao.

Ili mtu afikie mafanikio ya kweli ni lazima maisha yake yaongozwe na kanuni sahihi zinazompeleka katika kufanikiwa. Tunaposema *"kanuni sahihi"* tunamanisha mambo muhimu yanayoongoza tabia na mienendo ya mtu ambayo yakizingatiwa yana nafasi ya kumletea mafanikio. Maisha ya kubahatisha yasiyoongozwa na kanuni yoyote hayana uwezo wa kutuletea mafanikio. Hatupaswi kutegemea kwamba mafaniko yatatujia kibahababahati tu. Neno la Mungu linatufunulia kwamba Mungu hataki tuishi maisha ya kubahatisha bali anataka tuwe na hakika na mambo tunayotarajia maishani. Ndipo aliposema katika NENO lake;

***"Mwenye haki wangu ataishi kwa imani"; Ebr. 10:38*.**

Hii inamaanisha mtu anayetaka mafanikio anapaswa kuishi akiwa na hakika ya mambo anayotarajia maishani na akiona wazi mambo ya mbeleni yasiyoonekana. Kama kijana, unapaswa kuishi kwa imani kwa kuruhusu NENO la MUNGU likuongoze kuyaona mafanikio ya maisha yako, ambayo bado hayajadhihirika kwa macho.

Ili kuweze kusoma zaidi bonyeza........... **Buy Now**